# DARASA LA NNE

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

---

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

___**1**___ yangu, ambaye ndiye dada wa baba, alipenda kutusimulia ___**2**___ tamu. ___**3**___ alikuwa mzee sana kuliko mzazi wangu. Labda alizaliwa ___**4**___ ya baba kwa sababu baba yangu hajazeeka sana.

Kila ___**5**___ shule mimi nilipenda kwenda kwake ili nisipitwe na mambo ___**6**___. Lakini kuelekea mwisho ___**7**___ mwaka jana yeye ___**8**___ ugonjwa ___**9**___ unaoletwa na konokono. ___**10**___ ni ugonjwa ambao humfanya mtu kutokwa na damu ___**11**___ .

Tulipofunga shule ___**12**___ mwezi wa ___**13**___ mwishoni mwa mwaka, tulisafiri na mama yangu kwa gari letu ___**14**___ hadi huko. Nililia kwi kwi kwi nilipoambiwa kuwa alikuwa ameaga ___**15**___. Sitaisahau siku hiyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Shangazi | B. Nyanya | C. Halati | D. Mjomba |
| **2.** | A. mambo | B. hadidhi | C. stori | D. hadithi |
| **3.** | A. Yule | B. Mimi | C. Yeye | D. Wewe |
| **4.** | A. mbele | B. katikati | C. juu | D. nyuma |
| **5.** | A. tumefunga | B. tulipofunga | C. tufunge | D. tukifungua |
| **6.** | A. mzuri | B. mazuri | C. nzuri | D. hii |
| **7.** | A. ya | B. za | C. wa | D. mwa |
| **8.** | A. aliungua | B. aligojeka | C. aligonjeka | D. aliugua |
| **9.** | A. mhatari | B. baya | C. hatari | D. ubaya |
| **10.** | A. Huu | B. Hii | C. Haya | D. Hili |
| **11.** | A. nyingi | B. mingi | C. wingi | D. kingi |
| **12.** | A. letu | B. yetu | C. chetu | D. vyetu |
| **13.** | A. Januari | B. Oktoba | C. Disemba | D. Aprili |
| **14.** | A. lizuri | B. nzuri | C. mzuri | D. zuri |
| **15.** | A. dunia | B. safari | C. njia | D. Mungu |

***Kuanzia swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16. Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi.**
Tembo ________ amewapendeza watalii.
A. nono B. wanono
C. mnono D. wanene

**17. Tumia kiashiria sahihi kujaza pengo.**
Barabara ______ imewekwa lami.
A. hili B. hizi
C. hii D. huu

18. Kifaa cha kukunia nazi huitwa:-
A. mbuzi B. seredani
C. bilauri D. kinu.

19. Mkulima __________ mimea dawa baada ya kupalilia.
A. alivuna B. alinyunyizia
C. alipanda D. alifyeka

**20. Tegua kitendawili kifuatacho.**
Nikitoa naongeza.
A. Mbegu B. Nywele
C. Jua D. Shimo

21. Chagua sentensi inayoonyesha nafsi ya tatu.
A. Wewe hutaadhibiwa.
B. Wao wanashindana vyema.
C. Sisi tuna ng'ombe watatu.
D. Mimi hula kwa pupa.

**22. Fumbua fumbo lifuatalo.**
Jogoo wangu hutaga mayai mawili kila siku. Je, atataga mayai mangapi kwa siku tano?
A. Kumi B. Matano
C. jogoo hatagi D. Jogoo huzaa

23. Mtu hunywa maji ili:-
A. akate kiu B. akate kamba
C. aoshe koo D. akate tamaa.

**24. Kanusha sentensi ifuatayo.**
Kamba ya mbuzi inakatika.
A. Kamba ya mbuzi haikukatika.
B. Kamba ya mbuzi haitakatika.
C. Kamba ya mbuzi haijakatwa.
D. Kamba ya mbuzi haikatiki.

**25. Kamilisha:**
Chausiku ame ______ kata mwenyewe.
A. m B. ji
C. ni D. tu


26. Mmea wa mhindi huzaa:-
A. wahindi B. punje
C. mahindi D. kihindi.


27. Tunasema mawe mangapi na magari_______?
A. magani B. ligani
C. gani D. migani

28. Alama [ , ] huitwa:-
A. kipumuo B. nukta
C. kiulizi D. kikomo.

**29. Kamilisha:**
Mjukuu - kitukuu - __________
A. kilembwe B. kitujuu
C. kisuguu D. mtukuu

30. Chagua umbo la kopa.

A.


B.


C.


D.


***Soma kifungu kifuatacho kisha ajibu maswali 31-40.***

Swara mmoja alikuwa porini akila nyasi bila wasiwasi. Alikuwa ameamua kujitenga na wenzake ili atafute nyasi nzuri kwa sababu zilikuwa zimekauka. Alipokuwa akiendelea kula, aliona shimo mbele yake na akasimama ili asitumbukie ndani. Kando ya shimo hilo kulikuwa na mti mkubwa. Jambo ambalo swara hakujua ni kuwa juu ya mti huo kulikuwa na chui. Chui huyo alikuwa amemwona swara na akafurahi sana.

Swara aliposimama aliona nyasi nzuri upande ule mwingine wa shimo. Chui naye alianza kujiandaa ili amrukie swara yule na kumfanya kitoweo. Mara huyooo! Chui aliruka lakini kwa bahati mbaya, swara alikuwa asharuka kwenda upande mwingine wa shimo ili azipate nyasi nzuri. Chui alimkosa swara na tumbwi! Alitumbukia ndani ya shimo lile refu na akapotelea ndani.

Swara alishtuka aliposikia sauti ya kuanguka kwa kitu. Alirudi kwenye shimo lile kujua chanzo cha sauti ile. Alipochungulia ndani kwa makini, alimwona chui akihangaika. Mara alipiga mbio na kupotelea kichakani kwa hofu kubwa. Chui naye alibaki mle shimoni akipiga kelele za maumivu. Kwa kuwa hakuna mnyama yeyote aliyekuwa karibu, chui aliteseka kwa siku kadhaa na mwishowe akafa njaa.

---

**31.** Swara alikuwa porini akifanya nini?
- A. Akiwinda.
- B. Akiiba nyasi.
- C. Akitafuta maji.
- D. Akila nyasi.

**32.** Ili apate nyasi nzuri, swara aliamua:-
- A. kwenda peke yake
- B. kuruka mtini
- C. kula majani
- D. kujiunga na wenzake.

**33.** Swara alipoona shimo mbele yake:-
- A. alitumbukia ndani
- B. aliruka
- C. alisimama
- D. alitoroka.

**34.** Kulikuwa na _______ kando ya shimo.
- A. shimo kubwa
- B. chui
- C. nyasi nzuri
- D. mti mkubwa

**35.** Mbona chui alifurahi alipomwona swara?
- A. Alijua amepata chakula.
- B. Swara alikuwa rafiki yake.
- C. Swara alimchekesha sana.
- D. Alitaka kujaribu kuruka ndani ya shimo.

**36.** Chui aliporuka:-
- A. alimkamata swara
- B. alikufa
- C. alianguka shimoni
- D. alipata nyasi nzuri.

**37.** Chui na swara ni:-
- A. ndugu
- B. marafiki
- C. wapenzi
- D. maadui.

**38.** Swara hula nyasi naye chui hula:-
- A. maji  B. nyama
- C. udongo  D. matawi

**39.** Ni kwa nini swara alipiga mbio alipomwona chui ndani ya shimo?
- A. Aliogopa.
- B. Alikuwa na furaha.
- C. Kwenda kutafuta usaidizi wa kumwokoa chui.
- D. Nyasi zilikuwa zimekauka.

**40.** Mwishowe, chui aliteseka na kufa kwa:-
- A. shimo
- B. njaa
- C. hasira
- D. maumivu.